# Miundombinu wezeshi kwenye urejelezaji itatatua kero ya taka

**Na Halfani Chusi**

TANZANIA inaweza kudhibiti na kufikia azma ya taka sifuri kwa kufanya urejelezaji na kuweka miundombinu wezeshi ya uchakataji taka.

Mkurugenzi Mtendaji wa taasisi inayojihusisha na udhibiti wa taka nchini ya Nipe Fagio, Anna Rocha aliyesema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa Mkutano wa Kimataifa wa Miji ya Taka Sifuri uliokutanisha wadau mbalimbali.

Alisema kuwa hivi sasa Tanzania inafanya vizuri katika udhibiti wa taka kutokana na baadhi ya mikoa kuanza kutekeleza mfumo wa taka sifuri.

Alitaja mikoa hiyo kuwa ni pamoja na Arusha, Dar es Salaam, Tanga na Zanzibar, akisisitiza lengo la mkutano huo ni kujadiliana na kupeana elimu na namna ya kuifikisha katika mikoa mingine.

Alisema katika mkutano huo wawakilishi kutoka mikoa mingine nchini walikubali kupeleka elimu hiyo katika maeneo yao, ili kushirikiana kwa pamoja kudhibiti taka kama ilivyokuwa kwa Zanzibar ambao wamefanikiwa kupitia mfumo huo.

Alisema mfumo wa taka sifuri utasaidia kuifanya nchi kuwa safi, kuongeza ajira kwa vijana, kupata kipato kupitia faida zitakazopatikana kutokana na urejelezaji ikiwamo kuuza mbolea na chakula cha kuku.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Serikali za Mitaa Zanzibar, Mahmoud Mussa alisema utekelezaji mpango wa taka sifuri visiwani humo unalenga kuviweka safi visiwa hivyo.

Mratibu wa Miradi ya Ufadhili kutoka Benki ya Dunia (WB) kwa kushirikiana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini nchini (TARURA), Humphrey Kanyenye aliitaka jamii kushiriki na kutekeleza lengo la taka sifuri lililowekwa.

"Tuna uwezo wa kupunguza taka kwa kutumia vikundi mbalimbali vilivyopo kwenye jamii zetu kwa kukusanya, kuchakata na kupata mbolea inayoweza kutumika katika kilimo, viwavi kwa ajili ya chakula cha kuku hivyo sisi kama TAMISEMI na TARURA wenye Miradi inayoendelea hasa katika Mkoa wa Dar es salaam ujuzi huu umetuongezea faida nyingine," alisema Kanyenye.

Alisema kuwa kupitia Mradi wa Uendelezaji Jiji la Dar es Salaam (DMDP) wameanza na Nipe Fagio na kwamba mpango waliona kwa sasa ni kuanzisha mfumo wa usimamizi wa taka ngumu.

"Hii njia wanayoitumia wenzetu wa mataifa mengine ni nzuri, na itatusaidia sana kutokana na elimu ambayo imetolewa pale Bonyokwa ni mfano mkubwa, wananchi wanakusanya taka na kuzigawa katika mafungu matatu kisha wanazilejeleza na zinazosalia wanazipeleka dampo.

"Mfumo wa taka sifuri unajumuisha kuzigawa katika makundi manne ambayo ni rejeshi, zile zinazooza, hatarishi na nyinginezo na kisha zinachakatwa na kurejelezwa kwa ajili ya kupata bidhaa mbalimbali kama vile mbolea na chakula cha kuku,"alisema.




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitazama mashine ya mionzi CT Scan, kabla ya kuzindua huduma ya mionzi katika Hospitali ya Rufani ngazi ya Mkoa ya Tosamaganga, mkoani Iringa, jana. Wengine ni Askofu wa Jimbo Katoliki la Iringa, Mhashamu Tarcisus Ngalalekumtwa (kulia), Mkurugenzi wa hospital hiyo, Padri Benjamin Mafaume (wa tatu kushoto) na (wa pili kushoto) ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Peter Serukamba. **PICHA: OWM**

# Japan kuunganisha vipuri vya magari nchini

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) imesema wafanyabiashara kutoka Japan wanatarajia kuanza kuunganisha vipuri vya magari nchini.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Latifa Khamis wakati akizungumza na waandishi wa habari kwenye mkutano baina ya wafanyabiashara wa Tanzania na Japan uliofanyika kwenye Viwanja vya Maonesho ya 48 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam (DITF), barabara ya Kilwa.

Mkurugenzi huyo alisema wafanyabiashara hao wameamua kuja kufunga vipuri vya magari nchini baada ya kuona Watanzania wengi wananunua magari Japan.

"Wamesema Watanzania tunanunua sana magari ya kwao, hivyo wameona kuna fursa na wanataka kuja kufungua kama sehemu ya 'shoe case' lakini kuunganisha vipuri vya hayo magari," alisema Latifa.

Katika mkutano wao huo uliokutanisha wafanyabiashara kutoka kampuni tisa za Japan na wafanyabiashara wa Tanzania, ukilenga kuangalia fursa zinazopatikana katika nchi hizo mbili, pia walikubaliana kushirikiana katika maeneo mbalimbali ya miradi ya uwekezaji.

Kwa mujibu wa Latifa, maeneo mengine ya kuwekeza wanayoangalia ni katika sekta za kilimo, uvuvi, teknolojia, sekta za kutengeneza bidhaa za kuhifadhi vyakula na usafirishaji.

"Na kwa sababu wafanyabiashara hawa wote wanashiriki kwenye maonesho haya, tunataka baada ya hapa tufanye tathmini," alisema.

Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa, alisema majadiliano yaliyofanywa na wafanyabiashara wa nchi hizo mbili ni muhimu kwa kuwa yatasaidia kutoa mwelekeo mzuri wa kushirikiana kwenye uwekezaji.

Alisema amefurahia kushiriki katika mkutano huo wa kujadili na kuangalia fursa mbalimbali katika eneo la biashara na uwekezaji.

"Haya mataifa mawili ya Tanzania na Japan yamekuwa yakishirikiana kwa kipindi kirefu na sasa tumeona tuje tujadiliane namna ya kuongeza nguvu zaidi kwenye sekta za uzalishaji, kwahiyo tumebadilishana uzoefu wa kibiashara.

"Historia ya nchi hizi katika ushirikiano inatupa moyo kuendelea kushirikiana zaidi katika maeneo muhimu hususani ya kukuza uchumi," alisema Misawa.

# Mfumo e-Mrejesho waipa Tanzania tuzo ya kimataifa

**Na Romana Mallya**

SERIKALI imesema ushindi wa tuzo ya Umoja wa Mataifa ya Ubunifu katika Huduma za Umma kwa mwaka 2024 'UN Public Service Innovation Awards' kupitia mfumo wa e-Mrejesho ni kielelezo cha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Mfumo huo umetambuliwa na umoja huo kama jukwaa linalowezesha serikali kukusanya maoni na malalamiko ya wananchi kwa njia ya kidijitali na hivyo kufanya uamuzi wa sera na utekelezaji kwa wakati.

Hafla ya utoaji wa tuzo hizo ilifanyika Juni 26 mwaka huu, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma ya Umoja wa Mataifa 'UN Public Service Week 2024' katika Jiji la Incheon, Jamhuri ya Korea.

Tanzania ilikuwa moja ya nchi mbili tu za Afrika zilizotunukiwa tuzo hiyo, nyingine ikiwa ni Afrika Kusini ambapo jumla ya nchi 73 wanachama wa Umoja wa Mataifa zilishiriki na mifumo 400 iliwasilishwa wakati mifumo 15 pekee ndiyo ilishinda tuzo mbalimbali ukiwamo mfumo wa e-Mrejesho.

Tuzo hizo zilitolewa na Naibu Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa katika Idara ya Masuala ya Kiuchumi na ya Kijamii, Li Junhua, pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani wa Korea, Lee Sang-min, na kupokewa na Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Xavier Daudi.

Mkurugenzi Mkuu wa e-GA, Benedict Ndomba, alisema kuwa tuzo hiyo inaonesha utambuzi wa mchango mkubwa wa mfumo wa e-Mrejesho duniani kama jukwaa huru linalounganisha wananchi na serikali katika kuboresha utawala wa demokrasia kupitia teknolojia.

Alisema mfumo huo unaruhusu serikali kukusanya malalamiko, maswali na maoni ya wananchi na kuyafanyia kazi kwa wakati na pia, unamwezesha mwananchi kutuma maoni yake bila kujulikana ikiwa mwananchi hatotaka kujulikana.

"Mfumo wa e-Mrejesho ni jukwaa huru kwani umezingatia faragha za wananchi ambapo kwa wale wasiopenda kujulikana wanapowasilisha maoni yao serikalini wanaweza kuwasilisha bila kujulikana, na hivyo kuhakikisha sauti za watu zote zinasikilizwa, hii inachochea utamaduni wa uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma," alisema.

Ndomba alisema mfumo wa e-Mrejesho ni hatua kubwa katika juhudi za e-GA za kujenga daraja kati ya serikali na wananchi.

Alisema ushindi wa tuzo hiyo unaonesha azma ya e-GA ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika utawala wa umma kupitia teknolojia inavyotekelezwa.

Alibainisha kuwa ikiwa mwananchi atakosea kuwasilisha malalamiko yake katika taasisi husika, mfumo wa e-Mrejesho unaruhusu kuyahamisha kutoka taasisi moja kwenda taasisi nyingine.

Pia alisema unamruhusu mwananchi kukata rufani kwenda ngazi ya juu ya taasisi ikiwa hatoridhika na majibu yaliyotolewa kuhusu alicholalamikia.

"Mfumo huu unasaidia kuongeza uwajibikaji, kwani lalamiko linapofika kwenye taasisi litaonekana ngazi zote za uongozi wa taasisi hiyo na kila ofisa aliyelifungua ama kulifanyia kazi ataonekana," alisema.

Pia alisema unafanya uchambuzi wa taarifa na kumwezesha Katibu Mkuu Ofisi ya Rais - Utumishi na Katibu Mkuu Kiongozi kuona malalamiko yaliyo wazi, yanayoshugulikiwa na yaliyokamilika kupitia 'dashboard' maalum," alisema Ndomba.

Machi 13 mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwataka viongozi wa umma kutumia Mfumo e-Mrejesho ili kupokea maoni ya wananchi kuhusu serikali na kutoa mrejesho kwa wananchi kupitia mfumo huo ili kuimarisha uwajibikaji kwa viongozi wa umma.

Wiki ya Huduma ya Umma ya Umoja wa Mataifa ni tukio la kila mwaka linaloadhimishwa kimataifa kwa lengo la kusherehekea thamani na umuhimu wa huduma ya umma kwa jamii na hujadili jinsi ya kuboresha utoaji wa huduma kwa umma duniani kote.